

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA MITIHANI  
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**621**

**KISWAHILI**

**Muda: Saa 3**

**Jumatatu, 7 Mei 2012 mchana**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A, maswali **mawili (2)** kutoka katika kila sehemu B na C.
3. Sehemu A ina alama 40, sehemu B na C zina alama 30 kila moja.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Toa maneno ya Kiswahili sanifu kwa istilahi zifuatazo:
  - (a) E-mail
  - (b) Television
  - (c) Computer
  - (d) Fax
2. Taja namna nne za upatikanaji wa zana za kufundishia na kujifunzia.
3. (a) Andika maana ya mtaala wa somo la Kiswahili.  
(b) Bainisha vifaa vitatu vya mtaala wa somo la Kiswahili kwa shule za msingi.
4. Eleza kwa kifupi mambo manne yanayoonesha umuhimu wa vitendawili katika jamii.
5. Ainisha vipashio vinavyounda neno "analima".
6. Bainisha matatizo manne ambayo yanaweza kumpata mwalimu anayeingia darasani bila kujiandaa.
7. (a) Eleza miambatano miwili ya stadi za lugha.  
(b) Bainisha manufaa mawili ya kusoma kimya.
8. (a) Eleza maana ya fasihi simulizi.  
(b) Bainisha mambo matatu yanayoonesha kwamba fasihi simulizi ni hai.
9. Toa maana ya istilahi zifuatazo:
  - (a) Shajara ya somo la Kiswahili.
  - (b) Mpango wa kazi.
  - (c) Jedwali la kutahini.
  - (d) Tathilitha
10. Kwa kutoa hoja nne, eleza kwa ufupi umuhimu wa upimaji katika mchakato wa ufundishaji.

### SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

11. (a) Taja aina tano za maneno na kwa kila aina ya neno tunga sentensi moja.
  - (b) Bainisha aina za maneno yanayojenga sentensi zifuatazo :
    - (i) Mtu mmoja amekunywa chai yangu.
    - (ii) Niliwakuta vijana wanne wanalima shamba.
    - (iii) Mwaka jana ulileta neema
    - (iv) Baba anasoma kitabu na mama anapika chakula
    - (v) Baba anavaa kizungu, mimi kichina.
12. (a) Kwa kutumia mifano, bainisha tofauti kati ya mofolojia na fonolojia.
  - (b) Eleza kwa kina tofauti nne zilizopo baina ya kusoma kimya na kusoma kwa makini.
13. Tunga shairi la kimapokeo lenye beti tano kuhusu "Uchaguzi Mkuu wa 2010".
14. Fafanua tofauti iliyopo kati ya barua za kikazi na barua za kirafiki.

### SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

15. Elezea kwa kina mambo matano utakayozingatia katika kuandika mwandiko wa kuunga.
16. Tathmini manufaa matano ya kutumia muhtasari wa somo la Kiswahili katika ufundishaji na ujifunzaji. Toa mifano kwa kila hoja utakayotoa.
17. Fafanua mambo matano ya kuzingatia wakati wa kuandaa Azimio la Kazi.
18. Chambua changamoto tano zitokanazo na matumizi ya runinga katika kufundishia somo la Kiswahili.